

**Dondoo za Mkutano wa Umma wa Wapanda Baisikeli Dar es Salaam
12 Aprili 2008**

Waliohudhuria

Ally Athuman Jumbe
Ally Saidi Mohamedi
Ally Saidi Mwishehe
Aseli Wilison
Elaine Baker
Filbert Mbecha
Frank Peter Rwechungura
Juma Ali Salehe Jongo
Kassim Bakari
Kibwana Mohammad Msiga
Lameck Charles
Paulo Atibu Hatibu
Ramadhani Rajabu Nyengo
Sudi Saidi Ramadhan

Uzinduzi wa Ofisi

Juma amefanya kazi kwa wiki mbili kusambaza barua kwa watu na mashirika kuwaalika kwenye uzinduzi wa ofisi. Shirika la wadereva wa dala dala limehama ofisi na ofisi ya Diwani Bomani ipo mbali Pugu basi Elaine atawasiliana naye kwa simu. Pia Elaine atampa barua Professor Rwebangira. Mwakilishi wa Ubalozzi wa Uholonzi alitumia email kusema atajaribu kuhudhuria.

Juma alifuatalia kupata kibali kutoka serekali ya mitaa kufanya uzinduzi na amewahi kukipata. Pia amewapa nakala kwa kituo cha polisi karibu.

Ally Athman alishughulika kupata hema kwa kuweka nje ya ofisi kwa ajili ya kivuli. Kukodi hema na kusafirisha ofisini itakuwa na gharama ya Tsh 30,000.

Jirani ya Ally Saidi Mohammed's anayeitwa Charles ambaye anakodisha spika alikuja kwenye mkutano na tulimpa Tsh 20,000 advance (Tsh 14,000 kutoka hela ya guta na Tsh 6,000 kutoka Elaine – atarudishwa hela yake).

Dominata alisema kwa simu kwamba atawasiliana na waandishi wa habari. Atakutana na Elaine wakati wa wiki.

Tulikubali ratiba kama ifuatayo: 1) malengo ya UWABA na sababu za kuanzisha UWABA na faida za baisikeli 2) historia na mafanyikio ya UWABA 3) malengo ya ofisi na aina za taarifa zinazopatikana ofisini 4) wageni wajitambulishe na kusema maneno 5) shukuru kwa wadhamini na maombi ya michango 6) kutoa zawadi kwa wanachama 7) kukata ribbon 8) photo na kuendesha baisikeli kwenye uwanja 9) shukuru na mwisho.

Tulikubali kwamba Ally Saidi Mwishehe atakutana na Juma saa moja asubuhi jumamosi kituo cha Argentina pamoja na guta ya chama na watachukua helmet kutoka kwa Elaine na t-shirts, jaketi za njano na vifaa vingine kutoka kwa Juma kuzileta ofisini. Ally Saidi Mohammed atakodi guta ningine kuchukua vifaa vya spika. Ally Athman atahakikisha kwamba hema imefika na imeandaliwa.

Kuandaa ofisi

Elaine alileta karatasi za documents mbali mbali – barua tulizotuma na tulizopokea, taarifa na takwimu kutoka intaneti na taarifa kuhusu miradi yetu na tuliziweka kwenye rafu. Atatafuta printer ya rangi ili kutayarisha taarifa za bao za tangazo na ataleta wakati wa wiki.

Mambo ya hela

Juma alitumia Tsh 1,000 kwa ajili ya bahasha na Tsh 5,000 kwa ajili ya kibali. Ally Saidi Mwishehe alileta Tsh 14,000 kwa ajili ya wiki mbili ya hela ya guta na hii ilitumikwa kwa kulipa advance ya spika. Juma sasa ana Tsh 20,000 ya hela ya UWABA. Elaine alitumia Tsh 19,000 kununua faili kwa ajili ya karatasi za ofisi na alichangia Tsh 6,000 kwa ajili ya spika basi atahitaji kurudishwa hela hizi. Elaine na Juma wataenda benki kuchukua hela kwa ajili ya matumizi ya uzinduzi.

Wamba Memorial Fund

Dr Osili kutoka Wamba Memorial Fund alijibu emails zetu na aliomba namba za akaunti ya benki ya UWABA na Elaine alitumia taarifa hii wiki moja iliyopita. Elaine ataendelea kufuatalia.